East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 2, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Dhima ya Matambiko katika Jamii ya Waturkana

*Hosea Lorot Gogong*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S. L.P. 1100 – 20300. Nyahururu, Kenya.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0001-6003-5051; Barua pepe ya mawasiliano: lorot.gogong@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*05 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Aina ya Matambiko, Wahusika na Vifaa, Dhima ya Tambiko.*

**IKISIRI**

Makala hii inabainisha kuwa jamii ya Waturkana hutekeleza matambiko aina tofauti tofauti. Aidha, matambiko hayo huwa na dhima kubwa katika jamii hiyo. Stadi hii ilichochewa na haja ya kupigania nafasi stahili ya fasihi ya Mwafrika hususan nafasi ya matambiko katika tamaduni ya Waafrika. Makala hii itabaini na kuthibitisha kuwa, Matambiko yana nafasi muhimu sana katika fasihi ya jamii ya Waturkana. Pia, utafiti huu utathibitisha ufasihi wa matambiko. Nadharia za uhalisiajabu zilimwongoza mtafiti kuchunguza suala la matambiko katika jamii ya Waturkana. Pia, nadharia ya utendaji ilimsaidia mtafiti kuchunguza suala la utendaji wakati wa kutambika. Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo. Data kuhusu aina za matambiko na dhima yake ilikusanywa kutoka maktabani na nyanjani. Ili kuafikia lengo kuu, mbinu mbalimbali za ukusanyaji data zilitumika ambazo ni mahojiano, usikilizaji, utazamaji na unukuzi daftarini. Sampuli ziliteuliwa kimaksudi, mtafiti alitumia mtindo wa sampuli azimiwa katika kuwateua wazee ishirini na saba (27), wazee wa kiume kumi na nane (18) na wa kike tisa (9) kutoka katika vijiji tisa ambazo ni Kaenyumae, Moru-lingakirion, Nagetei, Loreng, Nareng-munyen, Nakimak, Edos, Kapoong, na Kadokochini. Wazee wa kiume wawili na wa kike mmoja waliteuliwa kutoka katika kila Kijiji. Vijiji hivi vinapatikana kwenye kata ndogo ya Locher-emoit iliyoko kwenye kata ya Lochwaa-Ngikamatak, eneo la Kaunti ndogo ya Turkana Kusini kwenye Kaunti ya Turkana. Idadi kubwa ya wakazi wa Kaunti ya Turkana ni Waturkana. Isitoshe, umri wa wazee walioteuliwa ulikuwa kuanzia miaka hamsini na tano kwenda mbele. Kigezo cha umri kilitumika kwa sababu inaaminika kuwa wazee wa umri huo ndio wana tajriba katika mchakato mzima wa utekelezaji wa matambiko. Kwa mujibu wa Ramsay (2005), data zilizokusanywa kutokana na mahojiano zilichanganuliwa kwa kuzingatia uchanganuzi wa kithamano. Aidha, data za utafiti huu ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

utafiti huu ni kuwa jamii ya Waturkana hutambika na huwa na matambiko ya aina tofauti tofauti. Isitoshe, utafiti huu umesaidia kukusanya data kuhusu matambiko na kuzihifadhi katika maandishi, kwani mambo mengi ya Fasihi Simulizi ya jamii ya Waturkana bado yamehifadhiwa vichwani mwa watu kama sehemu ya kutunzia kumbukumbu.

**APA CITATION**

Gogong, H. L. (2022). Dhima ya Matambiko katika Jamii ya Waturkana. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 85-99. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992.

**CHICAGO CITATION**

Gogong, Hosea Lorot. 2022. "Dhima ya Matambiko katika Jamii ya Waturkana". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 85-99. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992.

**HARVARD CITATION**

Gogong, H. L. (2022) "Dhima ya Matambiko katika Jamii ya Waturkana", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 85-99. doi: 10.37284/jammk.5.2.992.

**IEEE CITATION**

H. L. Gogong "Dhima ya Matambiko katika Jamii ya Waturkana", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 85-99, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Gogong, Hosea Lorot. "Dhima ya Matambiko katika Jamii ya Waturkana". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 85-99, doi:10.37284/jammk.5.2.992.

## UTANGULIZI

Makala hii imetokana na Utafiti kuhusu nafasi ya matambiko uliofanywa na mwandishi wa makala hii mwaka wa elfu mbili na ishirini na mbili (2022) na kuwasilishwa katika Chuo Kikuu cha Laikipia katika Kitengo cha Uzamili ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili. Utafiti huo ulifanywa katika vitongoji vya Kaenyumae, Kapoong na Kadokochini kwenye Kata Ndogo ya Locher-emoit iliyoko katika Kata ya Lochwaa-Ngikamatak Kaunti Ndogo ya Turkana kusini. Makala hii imeshughulikia nafasi ya matambiko katika jamii ya Waturkana. Wikipedia, Kamusi huru inasema, Waturkana ni watu wa asili ya Nilote wanaoishi kaskazini magharibi mwa nchi ya Kenya na kwenye Gatuzi la Turkana. Ni eneo kame na kavu linalopakana na Ziwa Turkana upande wa mashariki na kusini kwao wanaisha Wapokot, Warendile na Wasamburu. Lugha ya Waturkana ni yenye asili ya Kiniloti ya Mashariki, hujulikana kama Kiturkana. Idadi ya Waturkana ni 1,016,174, kwa mujibu wa matokeo ya idadi ya watu waliohesabiwa nchini Kenya mwaka wa 2019. Waturkana ni wafugaji wa Ngamia, Ng'ombe, Punda, Kondoo na Mbuzi. Waturkana hutegemea mito kadhaa, kama vile mto Turkwel na mto Kerio. Mito hiyo inapofurika, mchanga uliobebwa na maji ya mto pamoja na maji hujaza maeneo wazi ya mto na maeneo hayo hulimwa baada ya mvua nzito. Kisa ambacho hutokea kwa nadra.

Katika Fasihi Simulizi zao, wao hujiita watu wa fahali ya kijivu ambayo ina nafasi muhimu katika historia yao. Inaaminika kwamba fahali wa kijivu alipotea kutoka katika nchi ya Wakaramoja. Shujaa wanane kutoka kwa kabila la Jie wakamfuata fahali huyo hadi kando ya mto uitwao Tarach uliyoko karibu na mlima wa Nayece. Walipofika kwa mlima Nayece, walimpata fahali huyo wa kijivu akiwa na nyanya aitwaye Nayece. Nyanya huyo aliwapokea mashujaa hao vizuri. Alipojitambulisha kwao aliwaeleza kuwa yeye pia alitoka katika nchi ya Wakaramoja na harakati za kuchuma matunda ya mwitu ndizo zilizomfikisha hapo. Shujaa hao walipendezwa na mandhari hayo kisha wakarudi Karamoja kuwaleta watu wengine wa jamii zao na mifugo wao. Shujaa (ngikiliok) hao walipofika, Nayece aliwagawanya katika vikundi viwili kulingana na ujio wao, vikundi hivyo ni Ngimonea na Ngichuro. Nyanya Nayece akawa ndiye mama ya Waturkana wote yaani Ngimonea na Ngichuro kwa mjibu wa Fasihi Simulizi ya Waturkana. (Wikipedia)

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

Korobe (2021) anasema Ngimonea na Ngichuro walijigawa katika vikundi mbalimbali ambazo ndizo koo za Waturkana hadi sasa. Vikundi vya Ngimonea ni Ngikwatela, Ngiyapakuno, Ngisiger, Ngijie, Ngibochoros, Ngiesetou, Ngisonyoka na Anyangataak. Ngichuro wakajigawa katika Koo hizi; Ngilukumong, Ngiwoyakwara, Ngikamatak, Ngibilae na Ngikebootok. Koo au ukoo ni jambo la muhimu sana katika maeneo ya Turkana kwani wanajamii wa Kiturkana wanatambuana kwa majina ya ukoo.

Barrett (1998), anadahili kuwa koo za Waturkana zina alama maarufu (ngimacharini) ambazo zinawatambulisha katika jamii nzima. Alama hizo ni Ngipucho, Ngitengor, Ngidoca, Ngimacarmukata, Ngingolereto, Ngitarapakolong, Ngikosomoroko, Ngikaleeso, Ngisiger, Ngiduya, Ngisalika, Ngiponga, Ngikatap, Ngilobol, Ngikateok, Ngirarak, Ngimedeo, Ngilelet, Ngimerpur, Ngikadanya, Ngikinom na Ngiteso. Alama maarufu za koo huwekwa kwenye mifugo ili kusaidia katika kutofautisha mifugo wa koo mbalimbali.

Masebo (2007), anasema kuwa tambiko ni sadaka inayotolewa kwa mwenyezi Mungu, miungu au mahoka, mizimu na pepo kwao binafsi au kupitia kwa mwenyezi Mungu wakati wa kusalia miungu. Ejeem (2021), Samuel (2019) na Mathew (2013) wote wanakubaliana kuwa Waturkana hutambika na tambiko hizo ndizo huelekeza jamii haswa mtu anapopitia hatua za maisha kama vile, kuzaliwa, jando, kuoa au kuolewa na kufa. Matambiko ya Waturkana hufanywa nyumbani, makaburini, kwenye miti mikubwa, milimani, mapangoni, na porini. Matambiko ya Waturkana yalitolewa na wazee maarufu waliopewa jukumu hilo. Matatizo yaliyoshindikana kwa mababu zetu yalipelekwa kwa miungu ili iwasaidie kuyatatua. Kitula na Catherine (2010) anadahili kuwa, neno matambiko linatokana na imani kuwa mababu waliofariki wana uwezo wa kuona matendo ya watoto na wajukuu wao walio hai. Inadhaniwa kuwa wanapokasirika, watoto hupata matatizo ya magonjwa, vifo na mabalaa mengine. Ili kupoza hasira zao huko walikolala basi hupikwa pombe na vyakula vinavyokwenda kumwagwa makaburini au kuliwa na waganga ambapo vitendo hivyo ndivyo matambiko.

Manu (2003), amebainisha aina mbalimbali ya tambiko ambazo huzingatiwa katika jamii ya Kiafrika. amesema tambiko hizi ndizo huelekeza jamii haswa mtu anapopitia hatua za maisha kama vile, kuzaliwa, jando, kuoa au kuolewa na kufa. Hatua hizo za maisha hufanyiwa matambiko kulingana na jamii husika. Waturkana kwa sababu ni wafugaji hutambika kwa kutumia wanyama (kama vile ngamia, ng'ombe, punda, mbuzi na kondoo), tumbaku na maziwa. Matunda ya mwitu wakati mwingine hutumika. Waturkana hushikamana na mila au desturi, ngoma za mashetani, mizuka na vinyamkera vyao kama alama ya kuwaheshimu na kuwaenzi mababu zao wa kale. Wamitila (2002), anasema kuwa dhana ya matambiko inatumiwa kuhusiana na jamii nyingi za Kiafrika kuelezea shughuli za utoaji wa kafara na sadaka. Matambiko yalikuwa na umuhimu na uzito mkubwa katika jamii za kijadi kuliko jamii za siku hizi. Kimsingi tambiko ni sanaa kwa kuwa shughuli zenyewe zilikuwa na ufundi wa aina fulani. Zilitendeka mahali maalumu na waliohusika walikuwa watu wa umri fulani na maalumu. Jamii ya Wasambaa bado wanashiriki kwa ndani sana mambo haya ya matambiko na kuna sehemu maalumu za kufanya shughuli hizo za utoaji sadaka.

Mtafiti alichagua mada ya utafiti huu baada ya kufanya utafiti wa kina kuhusu yaliyoandikwa juu ya ufasihi wa matambiko. Mtafiti aligundua kuwa mpaka sasa kumekuwa na mjadala baina ya wanazuoni hususani wa fasihi kuhusu ufasihi wa tambiko. Mjadala huo umeibuka kwa lengo la kuhoji juu ya ufasihi uliopo kwenye tambiko na hata kudadisi ikiwa tambiko ni kipera cha fasihi au la (Samwel, 2013, 2015; Mulokozi, 2017). Samwel (2013), anatoa mtazamo wake kwa kueleza kuwa kinachochukuliwa kuwa ni fasihi katika tambiko ni maneno, yaani lugha ya kisanaa iliyotumika, manuizo pamoja na nyimbo na si matendo matupu yasiyo na maneno. Mtega (2021), alifanya utafiti kuhusu ufasihi wa tambiko kwa kuangazia Matambiko ya Wapangwa nchini Tanzania. Utafiti wake ulibaini yafuatayo: mosi, matambiko hutumia lugha teule ambayo huendana na muktadha wa kiutendaji pamoja na jambo linalowasilishwa. Pili, hutumia mbinu za kielimu-mitindo kama vile takriri, balagha, lugha ya picha, ishara na taswira mbalimbali ambavyo hutumika kwa shabaha maalumu. Vilevile, kuna matumizi ya mtindo wa kishairi katika kufikisha ujumbe. Mtindo huu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

huzingatia sifa za ushairi huru, uimbikaji, sentensi fupifupi ambazo hukidhi mawasiliano baina ya fanani na hadhira kwani huwa ni mtindo wa mazungumzo ambao huruhusu upande mmoja kusikiliza. Anaendelea kusema aidha, kuna matumizi ya nyimbo na tabano. Mwisho anasema kuwa kuna udhihirikaji wa sifa kuu ya Fasihi Simulizi ambayo ni utendaji wa kifasihi simulizi. Mtafiti anakubaliana na matokeo ya utafiti wa Mtega kuwa matambiko yanakidhi sifa za kuwa kipera cha Fasihi Simulizi.

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano katika kukusanya data kisha data hiyo ikachambuliwa mkabala wa kimaelezo yaani mkabala usio wa kiidadi. Stadi hii imebainisha kuwa; jamii ya Waturkana hufanya matambiko ya aina mbalimbali na hufanyika katika mazingira tofauti tofauti, kuna vifaa ambavyo hutumika katika kutekeleza zoezi la matambiko na pia matambiko yana dhima nyingi katika jamii ya Waturkana. Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yatathibitisha kuwa matambiko yana nafasi kubwa katika tamaduni ya jamii ya Waturkana. Kwa hivyo, utafiti huu una mchango mkubwa katika kuelewa uhalisia wa utekelezaji wa tambiko katika Fasihi Simulizi ya Waturkana na vigezo mbadala vinavyoweza kuzingatiwa katika uainishaji na uchanganuzi wake.

## MSINGI WA KINADHARIA

### Uhalisiajabu

Zamora (1995), anadahili kuwa nadharia ya uhalisia mazingaombwe ilianza mnamo mwaka wa 1925 na muasisi wake alikuwa mhakiki wa sanaa wa Kijerumani aliyeitwa Franz Roh. Dhana ya Roh ya nach-expressionism, magischer realism ikitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili inaashiria hali ya ajabu au mazingaombwe. Uhalisia ajabu unaeleza miujiza iliyomo kwenye uyakinifu wa kila siku. Msingi mkubwa wa nadharia hii ni usimulizi unaosimulia mambo au matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au unaokaribia na uhalisia, mwandishi anapaswa kuyamulika na kuyaakisi maisha katika nyanja zote kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Uhalisia unaongoza na kusisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usanifu mkubwa, uhalisia unapinga na kukataa aina yoyote ya majaribio. Nadharia hii ilimsaidia kwa kiasi kikubwa katika utafiti huu kwa kuwa matambiko yanazungumzia jamii na watu ambao kwa hakika waliishi na ni halisi pia yanazungumzia maisha halisi ya mwanadamu hususani Muafrika. Nadharia hii kimsingi inahusika sana na jamii ambazo zimechelewa hususani jamii nyingi za Afrika. Jamii ya Waturkana ni jamii ambayo kimsingi bado inaegemea sana mambo haya ya matambiko hivyo nadharia hii imekuwa kama mwanga katika utafiti huu kwani mambo ya matambiko ni mambo ya ajabu ajabu.

Mbatiah (2002:60) anasema: istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Kwa muhtasari, Franz Roh anasema: Uhalisiajabu ni uwasilishi wa ujumbe na hufichua hali ya kiroho na umazingaombwe katika chombo kwa kubainisha kudhihirika kwake na kukifanya zaidi ya kuwa halisi. Katika hali hii, uhalisiajabu hutuingiza katika ulimwengu wa kinjozi kwa kuwasilishwa kama “uhalisi”.

Mtafiti alitumia mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu kuchunguza aina za matambiko ya jamii ya Waturkana. Mihimili zifuatazo zilitumika: -

- Kueleza matukio ya kiajabu au ya kifantasia au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kuyafanya yaonekane ya kawaida. Huwepo hali ya kushangaza, kuduwaza na kuogofya. Mhimili huu utakuwa kama mwanga katika utafiti huu kwani mambo ya matambiko ni mambo ya ajabu na shughuli zake zenyewe ni za kimazingaombwe. Pia, watekelezaji wanawasiliana na viumbe ambao hawaonekani na hakuna ushahidi wa kisayansi wa kuthibitisha mawasiliano hayo japo kuna uhalisia lakini kwa kiasi fulani. Isitoshe, Lihraw (2010), anasema wawasilishaji wa nyimbo za jando walikuwa na uwezo usio wa kawaida kutokana na kupagawa na roho ya mila inayowapa nguvu za kiungu kuwasilisha mafunzo muhimu ya jando. Nguvu hizo huwafanya watumie maneno yasiyoeleweka

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

moja kwa moja katika miktadha yake maalum. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya ajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja inayofanana na yaonekana kama ya kawaida tu. Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezakana huwa madogo sana. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika.

- Mazingira huwa ni sehemu muhimu katika aina hii ya fasihi. Nyumbani, wanyama, misitu mikubwa, pango, kaburi na milima hurejelewa. Pia, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika kazi ya uhalisiajabu. Mhimili huu ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu suala la utekelezaji wa matambiko hufanyika porini/msituni, njia panda, kwenye miti mikubwa, kwenye mawe makubwa, makaburini, mapangoni, mtoni, ziwani, baharini, kwenye nyumba maalumu na mahali popote kutegemeana na aina ya tambiko.

- Wakati na mwanda (mahali/mandhari) hupanuliwa na kuwa na uhusiano mkubwa. Mpaka wa jadi baina ya nyakati huvunjwa kiasi kwamba matukio hayafuati kanuni ya uhalisi wa kiwakati. Mara nyingi mtazamo huu wa wakati unafungamana na suala la ndoto. Katika hali hii, mtunzi huweza kueleza kile kinachomkumba binadamu kabla ya kuzaliwa na baada ya kifo. Mwanda wa kisimulizi pia hupanuliwa. Huweza kuhusisha ulimwengu halisi, ulimwengu wa kidhanifu au ulimwengu wa kinjozi na maingiliano kati ya aina hizo tofauti huvunjwa. Mhimili huu ulitumika kuonyesha namna maghani ya matambiko ya jamii ya Waturkana huvunja mipaka ya nyakati. Kwa mfano fanani huelezea yanayohusu maisha ya mwanadamu kabla ya kuzaliwa na baada ya kifo kupitia maghani. Mandhari ya aina hii yameonyesha sifa ya utokaji kwenye ulimwengu halisi na kuingia kwenye ulimwengu wa kimawazo, kisha labda kurudi kwenye ulimwengu halisi. Pia, matambiko katika jamii ya Waturkana hufanywa katika vipindi maalumu kwani jamii ina mambo ambayo ni ya msimu na mengine ni ya dharura. Kwa mfano matambiko haswa ya ndoa hufanywa wakati mwezi umechomoza. Matambiko mengine hufanywa wakati mvua imenyesha.

- Uhalisiajabu unahusisha kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu. Hali mbalimbali kama uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na wenyeji/utamaduni huonekana zikiingiliana. Katika msingi huu matatizo yanayokabili jamii ya Waturkana yanayosababisha kufanyika kwa matambiko ni mambo halisia kabisa ila wanaopewa jukumu la kuyatatua au kuleta afueni dhidi ya matatizo hayo hapo ndio uhalisia wa ajabu unapokuja. Matambiko hutekelezwa nyakati mbalimbali mathalani wakati wa kuzaliwa, wakati wa jando wakati wa kuoa, wakati wa msiba na wakati wa tatizo.

## Nadharia ya Utendaji

Nadharia ya utendaji ilitumika kuhakiki suala la utendaji katika utafiti huu. Waasisi wa Nadharia ya utendaji kama vile Bauman (1975), Foley (1995) na Schechner (2013) wanashikilia kuwa wahakiki sharti wachunguze zaidi ya matini moja na kuhakiki utendaji unaoambatana na matini husika. Waasisi hawa wametambua na kupendekeza mihimili kadhaa inayosaidia na kutumika katika kuumba, kuwasilisha na kufasiri tajriba za wanadamu katika kazi ya kifasihi. Mihimili hiyo ni pamoja na imani kuwa uumbaji, uwasilishaji na upokezi wa Fasihi Simulizi unajengwa na: (i) Muundo wa tukio la kiutendaji kulingana na muktadha wa uwasilishaji. (ii) Utangamano wa fanani na hadhira wakati wa uwasilishaji wa fasihi. (iii) Mfanyiko wa kimawasiliano kulingana na kaida za utamaduni wa jamii inayochunguzwa.

Kwa mujibu wa Schechner (2013) utendaji ni tukio la aina yoyote ile linalowajumuisha hadhira pamoja na fanani wake kwa minajili ya kuigiza au kuonyesha tabia za wanadamu. Kutokana na maelezo yake, mipaka kati ya utendaji unaotokea katika kazi za kisanaa kwa upande mmoja na utendaji unaotokea katika shughuli za kila siku kwa upande mwingine ni wa kidhahania. Aidha, Matti (1993) anaona kuwa katika jamii za Kiafrika utendaji ulikuwa mojawapo wa kanuni za maisha ya kila siku. Ingawa maelezo ya wataalamu hawa hayaelekei kutenganisha baina ya utendaji wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

kifasihi na usio wa kifasihi. Faida moja tunayoipata kutokana na maelezo ya wataalamu hawa ni kuwa aina zote za utendaji zina dhima yake kwa wanajamii. Aidha, kutokana na Alembi (2002) pamoja na Mulokozi (2002), uhakiki wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika unapaswa kuzingatia namna fasihi hiyo inavyotendwa kwa kuwasilishwa mbele ya hadhira. Kwa ufupi, Mulokozi anaonelea kuwa msingi mkuu wa Nadharia ya Utendaji ni muktadha unaojumuisha fanani, hadhira, tukio na lugha.

Kwa upande mwingine, Alembi na Mulokozi wanatoa mawazo kuwa utendaji ni uti wa mgongo wa Fasihi Simulizi. Ndani ya utendaji huo, fanani huanzisha mawasiliano na pia hadhira hushiriki moja kwa moja katika kukamilisha mawasiliano kwa njia za kuuliza, kuelekeza, kuimba, na kujibu maswali ya fanani. Kadhalika, fanani anaweza kuupa nguvu utendaji wake kwa kutumia sio tu lugha ya maneno ya mdomo, bali pia hata kwa kutumia mitindo ya viziada lugha kama vile ishara za uso, mikono, kichwa na sauti wakati wa kuwasilisha sanaa yake (Okpewho, 1992). Katika jamii nyingi za Kiafrika, utendaji ulijumuisha shughuli za kawaida za kila siku kama vile kuzaliwa kwa mtoto, kupewa jina mtoto, kuoa na kadhalika. Viziada lugha ni mbinu ya mawasiliano inayotumia ishara za uso, mikono, uchezaji pamoja na sauti, hususan sauti za kimuziki. Kulingana na maoni ya mwanaisimu jamii Hymes (1974), nyenzo za kimawasiliano (lugha na viziada lugha), ujumbe na muktadha ni vijelezi muhimu vinavyojenga tukio la kiutendaji.

Mhimili mkuu wa nadharia hii umejengwa katika kuwapo kwa viashiria vya kiutendaji vya kifasihi simulizi (Bauman, 1975). Mihimili ya nadharia hii zilizotumiwa katika utafiti huu ni: - Matumizi ya lugha ya kisanaa kwa mfano, katika matambiko lugha inayotumika huwa na ubunifu ndani yake. Ubunifu huo hujidhihirisha wanapoanza kutoa maghani. Matumizi ya lugha ya kisanaa na kawaida ni mojawapo ya sifa pambanuzi za utendaji wa matambiko. Kutokana na mawasiliano ya utendaji, dhima ya matambiko ilibainika. Pili, kuwapo kwa hadhira na fanani. Kwa mfano, katika utendaji wa matambiko hadhira hujidhihirisha kupitia uwepo wa wahusika ambao ni dhahania. Wahusika hao dhahania ni kama vile Mungu, miungu, wahenga, mahoka na mizimu. Wahusika hawa hawajidhihirishi katika hali ya kimwili bali huwapo katika fikra za fanani ama watendaji na huaminika kuwa wapo, wanaona, wanasikia na wanajibu maombi. Tatu, kuwapo kwa matumizi ya lugha ya picha au ya kisanaa pamoja na matumizi ya viziada lugha. Mhimili huu hujikita katika kuchunguza vipashio mahsusi vya kisanaa kama vile ishara za viungo vya mwili (uso, mikono, miguu na kichwa), uchezaji dansi, maleba, ala za muziki pamoja na uigizaji.

Maghani ya matambiko uhusisha matumizi ya lugha za picha na matumizi ya viziada lugha ambazo viashiria vyake hufungamana na tukio pamoja na jamii husika. Nne, kuwapo kwa mbinu rasmi za kielimu-mitindo kama vile matumizi ya takriri, urari wa vina pamoja na uimbikaji. Uwasilishaji wa matambiko unahusisha pamoja na mambo mengine matumizi ya sauti na mapigo ya kimuziki kwa njia ya uganwaji au uimbaji na matumizi ya ala za muziki. Tano, kunakuwa na uzungumzaji maalumu (maghani) ambao hauendani na ule wa mazungumzo ya kawaida. Uzungumzaji huo huhusisha matumizi ya sauti ya kughani, yaani iliyo kati ya kuimba na kuzungumza. Aina hiyo ya uzungumzaji huashiria ufasihi wa matambiko. Sita, kuwapo kwa maneno yanayorejelea utamaduni na tukio fulani la jadi. Kwa mfano, utendaji wa tambiko uhusisha uteuzi makini wa maneno ambayo kwayo hutambulisha tukio na kufungamana na utendaji wa tukio hilo. Kutokana na ufungamanifu huo, matumizi ya maneno kama wahenga, mizimu, mahoka, mababu watukufu yanapotajwa katika utendaji wa tambiko huashiria utamaduni wa jamii husika. Mihimili ya nadharia ya utendaji ilimsaidia mtafiti katika utafiti huu.

## AINA YA MATAMBIKO NA MAZINGIRA AMBAYO MATAMBIKO HAYO HUTEKELEZWA KATIKA JAMII YA WATURKANA.

Mtafiti alifanya mahojiano na wazee ishirini na saba juu ya aina mbalimbali ya matambiko yanayotekelezwa katika jamii ya Waturkana. Stadi hiyo ilibaini kuwa Waturkana hufanya tambiko za aina tofauti tofauti katika mazingira mbalimbali kama zifuatazo: -

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

**Tambiko Linalohusiana na Kuzaliwa kwa Mtoto (Lokoit na Anapet)**

Tambiko hizi hufanywa mtoto anapozaliwa, Lokoit ni tambiko ambalo hujumuisha kuvunja mfupa wa mguu wa nyuma ya mbuzi. Wamama wakongwe humsaidia mama aliyejifungua kutekeleza tambiko hili. Tambiko hili hufanywa kuadhimisha mwisho wa kipindi cha kutengwa baada ya mama kujifungua. Kupitia tambiko hili mama aliyejifungua hupata uhuru wa kuanza kufanya shughuli za nyumbani. Pia wakati wa utekelezaji wa tambiko hili tumbaku hutupwa motoni, moto huo huwa ni moto uliowashwa kwa kupekecha kijiti kwenye gogo, wenyewe wanaliita moto mpya. Anapet ni tambiko ambalo hufanywa ili kutayarisha mbeleko ya kubebea mtoto, mbuzi huchinjwa kisha ngozi hutolewa kwa makini hatimaye ngozi hiyo hutumika kutengenezea mbeleko. Mbuzi anayechinjwa kwa tambiko hili lazima awe wa rangi nyeupe au kijivu, ngozi ya rangi nyeusi wala nyekundu haitumiki kamwe kutengenezea mbeleko. Mtoto anapoanza kutembea mkuu wa mbari humchinja mbuzi kisha tambiko la kutengenezea viatu likatekelezwa (akikep ng’amuk). Maghani na nyimbo hutolewa wakati wa utekelezaji wa tambiko hili.

**Tambiko la Jando (Asapan na Akinyonyo)**

Tambiko hizi hufanywa ili kubadilisha hadhi ya mtu kutoka kwa utoto hadi utu uzima. Asapan hufanyiwa mvulana, mvulana huyo hupewa mkuki atumie kumdungia beberu au ngoima kisha anaketishwa chini ya mti na kupakwa tuitumbo ya mbuzi huyo na kupewa mifupa ya uti wa mgongo wa mbuzi avunje huku akirudiarudia kusema maneno atakayoelezwa na msimamizi wake, anapewa nyama ale. Wazee hunywa damu na kula nyama ya Wanyama walioteketezwa hatimaye huwabariki wanajando kwa kughani. Hatimaye, kijana huyo huchukuliwa na msimamizi wake akaenda kwake, afikapo nyumbani kwa msimamizi wake mavazi yake yote huvuliwa kisha akavishwa mavazi mengine. Tendo hilo lina maana kuwa amevuliwa mavazi ya kitoto na anavikwa mavazi ya utuuzima. Nywele zake hunyolewa kwa kubakisha kidogo katikati ya kichwa na udongo hupakwa kwa ustadi katikati ya kichwa kwenye nywele zilizoachwa. Katika kipindi chote cha jando kijana huyo atakuwa akitema mate kisha anauliza swali juu ya kila kitu atakachokutana nacho kwa mfumo huu; anatema mate kisha anauliza hili ndilo gari? Hii ndio chakula? Haya ndio maji? Huu ndio mji? Huyu ndiye msichana? Huyu ndiye mzazi? Hapa ndiko kwetu? Maswali hayo ni ya balagha hayahitaji majibu. Baada ya wiki moja hurudishwa na msimamizi wake nyumbani kwao na afikapo hupokelewa na mamake kwa kumnyunyizia maji. Baada ya Tambiko hili hadhi ya mtu hubadilika na kuheshimika na jamii nzima. Akinyonyo pia ni Tambiko ambalo hufanyiwa msichana ili kubadilisha hadhi yake kutoka kwa usichana na kuwa mwanamke ambaye anaweza wajibika katika maswala ya nyumbani. Mbuzi huchinjwa kisha mwanamke huketishwa katikati ya boma kwenye ngozi ya ng’ombe mweupe kisha mavazi ya usichana huvuliwa na hatimaye huvikwa mavazi ya utu uzima au mwanamke. Wamama wazee kutoka kwenye mbari ambayo msichana huyo ameolewa ndio humfanyia Tambiko hili huku wakimfunza kunga za mbari ambayo ameingia.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

**Picha 1: Tambiko la jando (Asapan)**



**Matambiko Yanayohusiana na Harusi, Yaani Kuoa na Kuolewa (Akuuta)**

Harusi katika jamii ya Waturkana uhusisha matambiko mengi kama zifuatazo: -

***Tambiko la Eloto***

Jamaa ya bwana harusi huleta kondoo wanene wawili au zaidi kwa jamaa ya bibi harusi. Kondoo hao huchinjwa na huliwa na familia ya bibi harusi. Familia ya bibi harusi huwaandalia familia ya bwana harusi vyakula na mazungumzo ya kwanza juu ya mahari huanza. Kondoo wanapochinjwa ni ishara kuwa poza yenu imekubalika na mazungumzo baina ya jamii mbili husika yaendelee. Familia ya bwana harusi huketi upande wa mashariki ya boma ya wazazi wa bibi harusi wakati wote wa posa. Wakati wa mazungumzo hayo, lugha ya kimafumbo, jazanda, takriri, tashbihi na metali hutumika. Kwa mfano, msemaji wa familia ya bwana harusi ataanza kwa kusema, “mbuzi wangu alipotea na nilipofuata nyayo zake zilinielekeza hapa kwenu, naomba mnipe niende naye nyumbani”. Msemaji wa familia ya bibi hujibu pia kwa mafumbo akisema “mbuzi huyo yuko lakini amewekwa kwenye kilele cha mlima ulio mrefu, je mwaweza kukwea mlima huo?” Mbuzi anayerejelewa ni bibi harusi na mlima ni gharama ghali ya mahari. Maghani hutolewa kwa Mungu ikiongozwa na mzee mkongwe kabla ya mazungumzo hayo kuanza. Baada ya mazungumzo hayo, familia ya bwana harusi huialika familia ya bibi harusi kwao waje wapewe mahari kulingana na mapatano yao. Familia ya bibi huwasilisha ujumbe wao kwa familia ya bwana kupitia nyimbo. Iwapo mahari waliopewa haijawaridhisha wao huimba nyimbo za kuikejeli familia ya bwana harusi, mfano wa wimbo huo ni, mtoto wetu ameingia mahali peusi alikoingia sokwe mtu (…aloma ikoku nikirion nikolong alomari echom….). Iwapo mahari

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

waliopewa ni ya kuwaridhisha wanaimba nyimbo za shukrani na kuisifu familia ya bwana harusi.

***Tambiko la Emong / Ekuma***

Tambiko hili linahusu sherehe ya harusi. Watu wengi wa tabaka mbali mbali hukusanyika wakiwa wamejikwatua kwatu kwatu nyumbani kwa wazazi wa bibi harusi. Nyimbo, vigelegele, kuruka ngoma na kula nyama na vyakula vingine hutawala tambiko hili. Tambiko hili huchukua siku mbili mtawalia. Kwenye tambiko hili, ndume wawili wakubwa na wanene hudungwa mkuki, mmoja kwenye zizi na mwingine nje ya zizi nyumbani kwa wazazi wa bibi harusi. Bwana harusi ndiye huwadunga kuthibitisha kuwa amemwoa mke wake rasmi kwa mujibu wa mila ya Waturkana. Udongo mweupe hupakwa kwa maharusi hao pamoja na familia yao. Wakati huo maghani na nyimbo mbali mbali huimbwa huku vijana wakibeba nyama ya ng'ombe hao na kupeleka mahali pa kupikia. Jina la tambiko la ndume hao ni Emong au Ekuma, ndume hao huongeleshwa na wazee wasilete kisirani bali wafe bila kusumbua na jambo hilo hutimia. Pia mbuzi watatu huchinjwa na nyama yao hutayarishiwa nje ya boma kwa kuchomwa wala sio kuchemshwa. Nyama hii huliwa na wanaume wakati wa sherehe za harusi hiyo. Majina ya tambiko ya mbuzi hao ni Lomoni, Loyanae na Lomoru.

Aidha, mbuzi wengine wawili huchinjwa na nyama yao huchemshiwa ndani ya boma na kuliwa na wanawake. Majina ya tambiko ya mbuzi hao ni Nawama na Lokimul. Nawama inadhihirisha ngozi ambayo mama alimfunika msichana wake akiwa nyumbani na Lokimul inadhibitisha kionjo cha mahari ambayo msichana ameleta nyumbani. Baada ya sherehe ya harusi, tambiko la ng'akejen a ng'ibaren/ng'abuanakineta/Lokopir hufanyika. Familia ya bibi harusi huwapa mashemeji wao ndume mkubwa (anaweza kuwa ng'ombe au ngamia). Dume huyu huchinjwa mara tu baada ya bwana harusi na msafara wake kufika nyumbani kwao. Pia, tambiko la Akimuj hutekelezwa. Kwenye tambiko hili, matumbo ya dume huoshwa kwa maji mengi. Hii ni kutokana na imani kuwa tendo hilo humfanya mwanamke anayeolewa aweze kuzaa watoto wengi. Baada ya bibi harusi kushika mimba, tambiko la Eleu potis hutekelezwa. Mnyama anayetumika kutekeleza tambiko hili hutoka kwa mzazi wa bibi harusi. Ngozi ya mnyama huyo hutengenezwa na kutumiwa na mwanamke huyo akiwa mjamzito.

Nyimbo zinazoimbwa wakati wa sherehe ya harusi ya Waturkana hutekeleza wajibu mbalimbali madhalani; kushukuru familia ya bwana harusi kwa ukarimu, kuikejeli familia ya bwana arusi kwa uchoyo, kuwasifu wazazi wa bibi harusi, kujulisha familia ya bwana harusi na bibi harusi kwamba waimbaji wanahitaji nyama nyingine.

**Tambiko la Wakati wa Kifo (Akilur, Akuronor, na Apunyare)**

Hizi ni Tambiko ambazo hufanywa wakati wa kifo. Mzee anapoaga, maiti yake huzikwa ndani ya boma la mbuzi akiwa ameangalishwa upande wa mashariki kisha familia hufukia kaburi mchanga wakiwa wameangalia upande wa nyuma bila kulikabili kaburi moja kwa moja. Pia majani ya miti pamoja na mawe huwekwa juu ya kaburi. Mzee anapoaga, wajane wote huvua mapambo yao yote zikiwemo shanga kisha usiku huo wote wanalala kwenye nyumba ndogo moja huku miguu yao ikiwa imekunjwa na kufungwa. Vazi la wajane hao liitwalo abuo hupitishwa katikati ya miguu yao na kufungiwa kiunoni. Asubuhi wajane hao huvutwa nje na kuketishwa kwenye ngozi kisha wakanyolewa na kupakwa udongo mweusi. Mama akifa huzikwa ndani ya nyumba yake (Ekol). Tambiko la Akilur uhusisha familia ya mwendazake kunyolewa kwa nywele za upande wa mbele ya kichwa huku wakiwa wamepakwa tuitumbo ya wanyama waliochinjwa.

Tambiko la Akuronor pia hufanywa baada ya kumzika mwendazake. Ng'ombe, ngamia, mbuzi na kondoo wa boma hilo huelekezwa upande wa magharibi mwa boma. Wanyama kadhaa hudungwa kwa kutumia mkuki kuanzia mkubwa hadi mdogo. Anayewadunga wanyama hawa ni mzee wa mbari hiyo aliyepewa mamlaka na mbari hiyo kufanya kazi hiyo na anapoanza kazi hiyo huahikwa na jazba akitamka maneno yasiyoeleweka. Tambiko hili hufanywa kutuliza roho ya mwendazake. Pia ndume aliyekuwa fahari ya mwendazake pia huuliwa ikithamiriwa kuwa ataenda na Bwana wake katika ulimwengu wa kiroho. Apunyare hufanywa mwaka moja baada ya kifo cha mwendazake na hufanywa kumkumbuka mwendazake pia mbuzi wengi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

huchinjwa. Baada ya Tambiko la Apunyare, tambiko la Emo Ekile hutekelezwa, wazee wenye umri sawa na mwendazake hutafutwa na wakachinjiwa ndume mkubwa wakala kwa kuonyesha heshima kwa mwendazake. Wakati huo maghani na nyimbo hutolewa kwa kuigizwa.

**Tambiko la Utakazo (Amook)**

Tambiko hili hufanywa panapotokea jambo ambalo linahitaji utakazo katika jamii. Katika jamii ya Waturkana, inachukuliwa kuwa matendo mabaya ya wanajamii waliohai husababisha akina babu kukasirika na kusababisha mikosi au majanga katika jamii. Mahusiano kati ya mababu na wanajamii huharibika. Hivyo basi, uhusiano huu hurejeshwa kwa kupitia tambiko la Amook. Wakati wa tambiko hili, maghani pamoja na nyimbo hutolewa ikiongozwa na mzee wa umri wa makamu. Tambiko hili hufanywa kwa kumchinja mbuzi kisha tuitumbo hupakwa wanaofanyiwa tambiko hili kama ishara ya utakazo. Amook hufanywa kwa mazingira yafuatayo: -

- Hufanywa wakati mke amezini (elomit), haswa mke aliyeolewa rasmi kulingana na tamaduni za Waturkana. Kitendo hicho husababisha maafa kwa watu na mifugo hivyo basi Amook hufanywa ili kumtakasa mke na mshirika wake wa uzinifu.

- Kama mwanamme hana uwezo wa kumzalisha mkewe anafanya mpango kisiri na nduguye ili ashiriki kitendo cha ngono na mkewe apatapo mtoto Amook hufanywa ili mtoto awe wake familia.

- Wakati mume anaaga baada ya kumzika, tambiko hili hufanywa ili mke aweze kurithiwa na kakake marehemu.

- Wakati mtu anapigana na adui wake na amuue, akija nyumbani kabla hajatangamana na watu wengine hufanyiwa tambiko hili nje ya boma. Pia, tambiko la ng'ageran hufanywa kwa huyu mtu.

- Msichana aliyeolewa anaporudi nyumbani kwa babake hawezi ingia kwa boma kabla hajafanyiwa tambiko hili.

- Mtu anapogonjeka au mimba inapoharibika, tambiko hili hufanywa ili kutakasa na kuwatenga wahusika na magonjwa au bahati mbaya.

- Mwanamke aliyefanyiwa tambiko la akinyonyo hapaswi kuacha vazi lake la ngozi linalovaliwa upande wa mbele sehemu ya kiuno (adwel) liguze maji. Likiguza, tendo hilo litasababisha awe tasa au mtoto kufa baada ya kuzaliwa. Tambiko la Amook hufanywa ili kuzuia maafa hayo.

**Tambiko la Kutoboa Kichunguu (Akiped Akoomwa)**

Mila na desturi haimruhusu Mturkana kuoa ama kuolewa na mtu wa ukoo yake. Isitoshe, ni mwiko kushiriki tendo la ndoa na mtu wa ukoo yako. Mvulana anapokutana na msichana wa ukoo wake na kushiriki kitendo cha ngono kwa hiari au kwa kutojua, inapogunduliwa, wanashauriwa na kuonywa na jamii kisha tambiko hili linafanywa ili kuwaondolea nuksi hiyo na kuwatenganisha kabisa. Jambo hili lisipofanyika, jamii hiyo italaaniwa. Tambiko lahusisha kupakwa tuitumbo ya mbuzi kisha wakachimba kichuguu na kupitia kwenye shimo walilochimba kwenye shina la kichunguu hicho. Wazee wa ukoo hiyo hulaani kitendo hicho kisha huwaombea dua wahusika kupitia maghani.

**Tambiko la Kurejea (Awotun)**

Inaaminika kwamba wakati watu wanahama au kutembea nje ya boma wanaweza kutana na watu au vitu vinavyoweza kuwatia najisi na kusababisha nuksi katika maisha. Wakati mtu anarejea nyumbani kutoka alikokuwa anafanyiwa tambiko hili. Tambiko hili hufanywa kwa kutumia maji. Watu na mifugo hunyunyiziwa maji kabla ya kuingia langoni baada ya kuwa nje ya makao yao rasmi kwa muda mrefu. Hii hufanyika sana haswa kwa jamii hii wakati wa kuhama hama wakitafuta maji na nyasi. Mzee wa boma hufanya tambiko hili kisha mbuzi akachinjwa. Maghani huwa yanatolewa wakati maji yananyunyiziwa watu na wanyama. Pia, tambiko hili hufanywa wakati mke aliyeolewa anarudi nyumbani kwa wazazi wake, mamake humnyunyizia maji yaliyochanganywa na maziwa (erer).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

**Tambiko la Dua (Agata)**

Jamii ya Waturkana huamini kuwa uovu ukikithiri katika jamii miungu pamoja na mababu hukasirika na kusababisha majanga kama vile ukame, ajali, vifo vya ghafla, utengano katika jamii na magonjwa ya watu na mifugo. Tambiko la Agata hufanywa. Tambiko hili huhusisha kuchinja wanyama na kuwatolea akina babu na miungu (ng'akujo) haswa wakati jamii inahitaji mvua kutoka kwa Mungu (Akuj). Wazee hukutana sehemu ya kutoa kafara kisha hufanya maombi spesheli kwa miungu pamoja na mababu. Mmoja wa wazee aliye na umri ya juu kuliko wengine huongoza maghani hayo kisha wengine hushiriki kwa kujibu. Maghani hayo hutolewa ili kuondoa majanga kama vile ukame, magonjwa, mafuriko na ajali za aina yeyote. Sehemu maalumu huteuliwa na madhabahu yakaandaliwa kisha kafara ikatolewa juu ya madhabahu hayo.

**Tambiko la Uchunguzi (Aroun)**

Tambiko hili hufanywa na mganga, mganga hufanya uchunguzi au tafsiri ya matukio ambayo yametokea katika mazingira ya kutatanisha. Pia, tambiko hili hutumika kubashiri matukio yajayo. Tambiko hili hutekelezwa na mjuzi wa kuchunguza matumbo ya mnyama aliyechinjwa. Mbuzi huchinjwa kisha matumbo yakatolewa na mwenye kipawa cha kuchunguza kisha kufanyiwa uchunguzi na matokeo yakatolewa. Kwa mfano, ujumbe huwa wa heri kama vile ujio wa mvua au ujumbe wa shari kama vile uvamizi, magonjwa au ukame.

**Tambiko la Uganga (Amuronot)**

Tambiko hili hufanywa na mganga (Emuron) wakati uhusiano kati ya mtu au familia yake na Mungu imeharibika kutokana na matendo yake au matendo ya familia yake. Mbuzi huchinjwa na tambiko hili kutendeka ili kurejesha mahusiano mema kati ya mtu na Mungu (Akuj). Pia, tambiko hili hufanyika wakati mtu ni mgonjwa. Mganga humfanyia uganga ili aweze kupona. Mganga pia huweza kumchinja mbuzi kisha matumbo yake yakatolewa na kuangaliwa kwa ustadi na jumbe tofauti tofauti hutolewa kwa jamii nzima. Kwa mfano, ugonjwa, kuja kwa mvua, uvamizi, mafuriko, vita na amani. Aidha, mganga pia hufanya tambiko la kutega na kutegua mipango ya maadui (Ariwo). Tambiko hili hufanywa ili kutegua au kusambaratisha mipango ya kichawi ambayo adui hupanga ili kusababisha kifo, kumpumbaza mtu ili mifugo wake waibiwe, magonjwa, ajali au majanga katika jamii husika.

Tambiko hili linapotekelezwa jamii inaamini kuwa mipango hiyo itasitishwa na kuelekezwa kwa maadui waliopanga. Tambiko hili hutekelezwa baada ya tambiko la uchunguzi (Aroun). Shari yoyote itakayochunguzwa na kuonwa kwa jicho la uganga huteguliwa kiuganga kabla kutokea. Pia tambiko hilo hutumiwa kumtegea adui, mtego ambao utamnasa akili. Kwa mfano, adui hupumbazika na kujipeleka mwenyewe mikononi mwa aliyemfanyia tambiko hili.

**Tambiko la kubariki boma (Akiteremokin au Apiarete Anawi)**

Tambiko hili hufanywa kila mwaka ili kutoa shukrani kwa Mungu baada ya kubariki boma la anayefanya kwa mifugo wengi, afya ya mifugo na ya jamii nzima na baraka ya mvua. Kafara ya Wanyama hutolewa kwa Mungu. Udongo maalum hupakwa kwa wanajamii hao. Mzee mkongwe katika jamii ndiye huongoza jamii katika kutekeleza tambiko hilo. Aidha, Tambiko la ketema mate (akimaakin) pia hufanywa na mzee wa makamo ambaye hutumia maji kuwatemea watu katika jamii husika, mzee huyu hunywa maji kisha huwatemea anaowatambikia. Tambiko hili hufanywa ili kuwabariki wanajamii na kusababisha utulivu katika maisha yao. Pia wakati mtu anaenda sehemu ambayo ni hatari hufanyiwa tambiko hili la kutemewa mate ili afike aendako salama.

**Tambiko la Ibada kwa Miungu (Ngasenon)**

Tambiko la ngasenon hufanywa mlimani haswa karibu na njia ipandayo mlimani au ipitayo katikati ya milima. Katika tambiko hili tumbaku, majani mabichi ya mti wowote au jiwe hutumika. Jamii ya kitamaduni ya Waturkana wanaamini kuwa Mungu wao yuko kwenye ngasenon na unapopita pale unamuabudu kwa kumtupia tumbaku, jiwe au majani mabichi. Unapofanya tambiko hili safari yako inakuwa njema na yenye Baraka.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

## DHIMA YA MATAMBIKO KATIKA JAMII YA WATURKANA

Matambiko yana dhima nyingi katika jamii ya kabila la Waturkana. Mtafiti aliweza kuhojiana na wanajamii 27 ambapo waliohojiwa walikuwa ni wazee wenye umri wa zaidi ya miaka hamsini na tano. Matokeo ya mahojiano hayo yalibainisha kuwa matambiko ya jamii ya Waturkana yana dhima nyingi. Baadhi ya dhima hizo ni kama zifuatazo: -

### Dhima ya Kuitambulisha Jamii

Kila jamii huwa na mitindo yake ya kuwasilisha sanaa za fasihi ambayo huwa kitambulisho chake. Jamii huweza kutambulika kupitia utamaduni wake ambao huelezwa vyema zaidi kupitia Fasihi Simulizi mathalani nyimbo, ngano na maghani (M'Ngaruthi, 2008). Vilevile, visasili, mivigha na nyimbo mbalimbali huwa kati ya vipengele vinavyoitambulisha jamii husika. Jamii ya Waturkana hutumia lugha wakati wa kutekeleza matambiko na lugha hiyo. Huitambulisha jamii na kudhihirisha uhusiano wa kitamaduni uliopo kati ya wanajamii wake. Jamii husifika kutokana na sanaa yao katika Fasihi Simulizi kama vile maghani. Miktadha ya kitamaduni na kihistoria huongoza uteuzi wa lugha kwa msanii yeyote, kwani lugha husheheni mila, itikadi, amali, tabia na mawasiliano ya jamii husika (Wanjala, 2015). Nyimbo, maghani, maleba na miondoko ya aina mbalimbali inayotendeka wakati wa utekelezaji wa matambiko mbalimbali hutambulisha utamaduni wa Waturkana.

### Dhima ya Kurithisha Utamaduni, Mila na Desturi

Matambiko husaidia kuelimisha jamii kuhusu thamani za kijamii, historia, utamaduni na mtazamo wao kilimwengu kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Kwa njia hii, jamii husika huhamasishwa juu ya mawazo yanayohusiana na tamaduni na desturi za jamii husika ili jamii hizo zipate mwelekeo unaowabainisha wao mbali na jamii zingine (Mwiza, 2014). Aidha, matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa matambiko husaidia kuendeleza mila na desturi za jamii ya Waturkana kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Matambiko yana umuhimu mkubwa sana kwa sababu yenyewe ni kama njia ya kuwafundisha wanajamii jinsi ya kutatua matatizo yao kijamii. Kwa jinsi hiyo, mila na desturi za jamii husika huendelea kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa sababu wakati wa matambiko katika jamii ya Waturkana uhusisha wake kwa wanaume, wazee na vijana ambapo vijana huona jinsi wazee maalumu wanavyofanya, hivyo hata kesho wazee hao wasipokua basi vijana watafanya. Mila na desturi zinaendelezwa kupitia matambiko mbalimbali. Kwa mfano tambiko hufanywa mtoto anapozaliwa, anapoingia utu uzima, anapoolewa au kuoa na hatimaye anapoiaga dunia. Vijana hufunzwa taratibu za kufuata katika kutunza na kuendeleza mila na desturi za kabila la Waturkana. Louis (1995), anasema uhalisia ajabu unapaswa kueleweka kwa kadiri fulani kama mkabala wa kuuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka kati ya dhana, vitu au hali. Katika jamii ya Waturkana, ni ukweli kabisa kuwa matambiko ni chombo kikubwa cha kuendeleza mila na desturi za jamii hii. Matambiko huvuka mipaka ya dunia hii na kusongea mbali na kufikia upeo wa juu wa dunia nyingine ambayo kwao wanaamini ni kuzimu yaani sehemu maalumu zinakoishi roho za watu waliokufa hususani za wale waliotenda mambo mema. Na Waturkana wana imani kuwa matatizo ni matokeo ya kuchukia kwa mizimu.

### Dhima ya Kusuluhisha Matatizo katika Jamii

Matambiko hutumika kuleta suluhu ya matatizo katika jamii ya Waturkana. Kwa mfano, kama jamii imekumbwa na janga la aina yoyote, Mungu huombwa kupitia tambiko ainusuru jamii kutokana na janga hilo. Jambo hili latendeka jamii ikiwa na imani kuwa ni Mungu ndiye ana uwezo wa kukomesha janga lolote. Matambiko huiongoza jamii katika mapambano dhidi ya matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii husika. Kwa mfano, ukame, mafuriko, njaa, ajali na mambo mengine mengi. Kwa kupitia matambiko, jamii huongozwa katika kupambana nayo kwani unapotokea ukame na pengine wanajamii wanatumia vibaya rasilimali zilizopo kama misitu, kwa kupitia matambiko, wanapata ujumbe juu ya kutunza misitu au hata kutumia mito kwa shughuli maalumu na sio shughuli ambazo ni za kuharibu mazingira kwani kwa kufanya hivyo wahenga wanakasirika na kuwaletea matatizo hayo kama adhabu.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

Njogu na Wafula (2007), wanaeleza uhalisia ulitokana na matatizo yaliyokuwa yanawakabili watu. Matatizo hayo yaliwafanya watu kuanza kushutumu ulimbwende na matamanio ya kilimbwende yalikuwa ya kiusingizini (kinjozi) zaidi yakilinganishwa na shida na matatizo yaliyokuwa yanawakabili watu. Hapa, Wasambaa nao walikuwa wanakabiliana na matatizo yao ya kawaida kwa kutafuta suluhu kutoka kwa mizimu, miungu yao ambayo kiuhalisia nguvu hizo hazina nguvu ila kiajabuajabu mizimu na miungu ina nguvu sana hususani katika kutatua matatizo.

### Dhima ya Kuburudisha

Maghani yanayotolewa wakati wa utekelezaji wa matambiko ya jamii ya Waturkana huchukua sifa za ushairi. Aidha, nyimbo zenye ujumbe tofautitofauti huimbwa. Nyimbo na shairi kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi huburudisha jamii kupitia vipera vyake vya fasihi vinavyolenga aghalabu kutumbuiza, kufurahisha na kusisimua. Wakati wa kuwapasha watahiriwa tohara ya jando huwa ni wakati wa kuburudika kwa wanajamii wote pamoja na majirani na marafiki wanaofika kushuhudia tohara hii. Vilevile, watahiriwa ambao huwa wamefanya matayarisho kwa muda mrefu huburudika. Kwao, shughuli hii ya tohara ya jando huja mara moja tu katika maisha yao, hivyo, hubidi kuifurahia. Washiriki wote huburudika kwa kina kutokana na nyimbo na maghani yanayotolewa mathalani nyiso na mahali ya tohara hii. Kulingana na Lihraw (2010), watahiriwa walipewa mafunzo kabla ya wakati huu kuhusu namna ya kucheza kengele kwa sauti na midundo ya kujifurahisha na kukidhi mahitaji mbalimbali ya jando.

### Dhima ya Kujenga Mahusiano Mema katika Jamii

Mahusiano mema hudumishwa katika jamii ya Waturkana kupitia utekelezaji wa Matambiko. Utekelezaji wa Matambiko husaidia kujenga na kuimarisha mahusiano mema miongoni mwa wanajamii. Katika jamii ya Waturkana, ikitokea wanajamii wamekosana, kwa mfano, mme akimpata mkewe akiwa na mahusiano ya ngono na mwanamme mwingine, wazee huketi na kutoa suluhu ya mzozo huo kisha mwanamke aliyehusika hufanyiwa tambiko la utakazo (Amook). Pia, tambiko husaidia kuwaadhibu wanaoiasi mila na desturi katika tamaduni za Waturkana. Kwa mfano, yeyote anayeshiriki ngono na dadake au mtoto wa shangazi au mjomba, huadhibiwa kwa kutekeleza tambiko la kuchimba kichunguu na kupita ndani yake (akiped akoomwa).

Watu wa ukoo mmoja wakipatikana wakishiriki kitendo cha ngono, tendo hilo huchukuliwa kuwa laana kwa ukoo nzima. Isitoshe, mahusiano ya wanajamii na miungu ikiharibika kutokana na matendo mabaya ya wanajamii, tambiko hutekelezwa ili kuwatuliza mababu au miungu (akipeyore a ngikasiak). Matendo hayo hutendwa kwa mujibu wa uhalisiajabu. Haen (2005), anaelezea uhalisia mazingaombwe kwa kuchukua michoro iliyo na uhalisia kama picha ya kamera lakini iliyoibua hisia kwa kuchanganya uhalisia na ukosefu wa uhalisia. Wanajamii waliokoseana katika hali ya uhalisia hupata hofu ya ajabu na kuelewana na kuheshimiana katika hali ya kiajabuajabu. Tambiko hutumiwa kama chombo cha kumshukuru Mungu pamoja na mababu kwa ulinzi na baraka ambazo jamii imepokea mwaka huo. Ni tendo ambalo linatekelezwa kila mara katika tamaduni ya jamii ya Waturkana.

## HITIMISHO

Makala hii imebainisha kuwa: jamii ya Waturkana hufanya matambiko ya aina mbalimbali na hufanyika katika mazingira tofauti tofauti, kuna vifaa ambavyo hutumika katika kutekeleza zoezi la matambiko na pia matambiko yana dhima nyingi katika jamii ya Waturkana. Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwa matambiko yana nafasi muhimu katika tamaduni ya jamii ya Waturkana. Kwa hivyo, stadi hii ina mchango mkubwa katika kuelewa uhalisia wa utekelezaji wa tambiko katika Fasihi Simulizi ya Waturkana.

## MAREJELEO


Alembi, E. (2002). *“The Construction of the Abanyole Perceptions on Death through Oral Funeral Poetry.”* Tasnifu ya uzamifu, Chuo kikuu cha Helsinki.

Ampim, M. (2003). *Africa studies. Five major African initiation rites*. https://www.manuampim.com/AfricanInitiationRites.htm


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

Barrett, A. J. (1998). *Sacrifice and prophecy in Turkana cosmology*. Paulines Publications Africa.

Bauman, R. (1975). *Verbal Art as Perfomance*. New Jersey: Blackwell Publishing.

Ejeem. C. (2021, December 10). Turkana Women Rite Of Passage(Akinyonyo). Turkana Diary. https://turkanadiary.com/turkana-woman-rite-of-passageakinyonyo/

Foley, M. (1995). *Singer of Tales in Performance Voices in performance and text*. Bloomingon: Indiana University Press.

Haen, D. (2005). Magic realism and Postmodernism: Decentering Privileged Centers. Zamora Lois Parkison & Wendy Faris (Eds.) *Magic Realism: Theory, History, Community*. Durham & London: Duke University Press. pp. 191-208.

Hymes. D. (1974). *Foundations in sociolinguistics. An ethnographic approach*. Philadelphia. University of Pennsylavia Press.

Oxford University Press. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* . Oxford University Press. Kenya. Kirama, Kh. (1953) *Habari za Wakilindi,* Vuga Press.

Kitula, K. & Catherine, N.M.K (2010) *Misingi ya Fasihi Simulizi*Kenya litearure Bereau.

Korobe, B. (2021). The Southern Limits of the Turkana: Ethno-Cultural History, Origin, Migration, and Settlement of three Pastoral Neighbors - the Turkana, Pokot, and Samburu 1700 – 2020. Journal of African Interdisciplinary Studies, 5(5), 35 – 63

Korobe, B. L. (2021). Turkana Kinship System and Social Structure: an Analysis of the Family, Patrilineage, Patriclan, and Phratric Organization. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, *5*(10), 99-136.

Lihraw, D. (2010). *The Tachoni Peoples: History, Culture and Economy*. Entrepreneurship Development Institute (EDS), Nairobi

Louis, Z. (1995). *Magical Realism: Theory, History, Community*. Duke University Press.

M'Ngaruthi, N. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni: Kitabu cha Walimu na Wanafunzi (Shule na Vyuo)*. The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Masebo . A. (2007) *Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita*, Nyambari Nyangwine publishers.

Matti, M. (1993). "*Sanaa za maonyesho za Kiafrika za jadi: Mfano wa Tohara ya Watharaka" Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa*. Chuo Kikuu Cha Moi.

Mbatiah, S. (2002). *Hatua za maendeleo ya uhakiki wa fasihi ya kiswahili nchini Kenya a publication of the National Kswahili association; Akimeru fork tell*. Chuo Kikuu cha Nairobi

Mtega, W. (2021) Ufasihi wa matambiko: Uchunguzi wa matambiko ya Wapangwa: Kioo cha lugha. *Jarida la taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.

Mulokozi, M. (2002). *The African Epic Contoversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers

Mwiza, P. (2014). *Umuhimu wa Fasihi Simulizi katika jamii. Kutoka petermwiza Blogspot.com na Mwaka wa Kogwa*. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character, and Continuity*. Bloomington: Indiana University Press.

Ramsay, H. (2005, Winter). *Preserving the Haida Language*. Canadian Teacher Magazine. Retrieved October 1, 2010, from http://www.canadianteachermagazine.com/ctm_first_nations_education/winter05_preserving_haida_language.shtml

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.992

Roh, F. (1925). *Nach-Expressionismus: Magischer Realismus: Probleme der neuesten europäischen Malerei*. Klinkhardt & Biermann.

Samuel, D. (2019). *Appreciating Asapan- Turkana initiation ceremonies*. St John College at the University of oxford in Uk.

Samwel, M. (2013). *Tamthiliya ya Kiswahili: Kutoka Miviga ya Kidini Hadi Filamu*. Dar es Salaam: MEVELI Book Publishers.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Book Publishers.

Schechner, R. (2013). (3rd ed). *Performance Studies: An Introduction*. NewYork: Routledge.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi na Vipengele vyake*. Nairobi, Kenya: Phoenix publishers Ltd.

Wanjala, W. (2015). *Mwingiliano tanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kongwa.* Tasnifu ya uzamifu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta Nairobi.

Zamora, Lois Parkinson. (1995). Magical Romance/Magical Realism: Ghosts in U.S. and Latin American Fiction. In Lois Parkinson Zamora and Wendy B. Faris (Eds.), *Magical Realism: Theory, History, Community* (pp. 497–550). Durham: Duke University Press.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.